SWAHILI

# MAP OF SUCCESS

## RAMANI YA MAFANIKIO

MAOMBI ABEL CHAGAMBA

YALIYOMO

UTANGULIZI ....................................................................................................7

FALSAFA NO 1 ..................................................................................................8

mafanikio yoyote yale yana anzia kichwani kwako .........................................................8

FALSAFA YA 2..................................................................................................19

usiishi ndoto ya wazazi wako au jamii inayokuzunguka.................................................19

FALSAFA NAMBA 3 ...........................................................................................30

usitafasiliwe na jana yako ...................................................................................30

FALSAFA NAMBA 4 ...........................................................................................40

you will lose your teeth when you grow old (utapoteza meno ukiwa mzee)..................40

FALSAFA NAMBA 5 ...........................................................................................44

usipovunja mazoea ukiwa kijana utazeeka na hayo mazoea..........................................44

FALSAFA NAMBA 6.............................................................................................46

unahitaji kichwa ambacho kimetulia kwa gharama zote................................................46

FALSAFA NAMBA 7 ...........................................................................................51

kuwa busy kunafanya upoteze muelekeo wa fikra (perspective)...................................51

FALFASA NO 8...................................................................................................58

the law of season...............................................................................................58

FALSAFA YA 9...................................................................................................65

safari moja huanzisha nyingine...........................................................................65

FALSAFA YA 10.................................................................................................74

ni nini ulichonacho mkononi mwako. (sehemu bora ya kuanza safari yako)................74

FALSAFA NAMBA 11..........................................................................................81

kanuni ya kioo (mirrow principle).........................................................................81

FALSAFA NAMBA 12 .........................................................................................88

is this all you can do?........................................................................................88

FALSAFA NAMBA 13 .........................................................................................92

leverage on your result .....................................................................................92

**©Maombi A. Chagamba**


**Simu: +255713999596,**


**+255752102169**

**WhatsApp:**

**+255713999596**

**Email wiseinvestorr@gmail.com**


JINSI YA
KUWEKEZA
UTT AMIS
MAOMBI CHAGAMBA


MIKAKATI MIWILI YA KUWEKEZA KATIKA SOKO LA HISA
two strategies
MAOMBI CHAGAMBA


JINSI YA KUWEKEZA KATIKA SOKO LA HISA (DSE)
MAOMBI A CHAGAMBA


MAMBO 9 UNAYOTAKIWA KUJUA KUHUSU KUNENA
KWA LUGHA
Na jinsi unavyoweza kuanza kunena kwa lugha
Maombi Abel chagamba


UTT AMIS KWA
MTU
MWENYE HARAKA
MWONGOZO MWEPESI WA KUWEKEZA UTT AMIS
MAOMBI ABEL CHAGAMBA

HAKI MILIKI

Haki zote zipo chini ya MAOMBI ABEL CHAGAMBA, hairuhusiwi kunakiri, kudurufu, au kutumia sehemu ya kitabu bila idhini ya mwandishi.

# FALSAFA YA 2

## USIISHI NDOTO YA WAZAZI WAKO AU JAMII INAYOKUZUNGUKA.

Kuna watu katika maisha hawajawahi kuwaza nini wanataka katika maisha au wanataka maisha yao yaweje

Kitu ambacho wanafanya ni kitu ambacho wameambiwa au wamekua wakifundishwa kufanya toka wakiwa watoto na wazazi wao au jamii inayowazunguka  hawajawahi kuwaza wao kama wao (to think for themselves).

Ijapokuwa watu duniani tuko takribani bilioni 8, hakuna watu wawili wenye alama za vidole ambazo zinafanana na hakuna watu wawili ambao wana fanana ila cha kushangaza ni kuwa kila kukicha jamii inayotuzunguka inatufundisha nini iwe ndoto yetu katika maisha ilihali sisi tuko tofauti na wao. Au kwa kifupi tunafundishwa namna sawa ya kufikiri ilihali sisi tuko tofauti.

## ULIMWENGU UNAOBADILIKA

Miaka kadhaa iliyopita nilisoma katika jarida moja ya kuwa elimu (knowledge) huwa inaongezeka mara mbili kila baada ya miaka 2 hii ina maana ukisoma kitu leo kuna uwezekano wa kuwa baada ya miaka 2 hicho kitu kinaweza aidha kisiwe kweli tena au kikawa kimepitwa na wakati kwa hiyo inapotokea vijana wa leo tunaongozwa na ndoto za wazazi wetu ambao waliishi katika karne iliyopita kuna uwezekano wa kuwa tutaachwa kimaendeleo na kifikra na watu wa mataifa mengine.

ni ukweli usiopingika ya kuwa maisha ambayo wazazi wetu au mababu zetu waliishi ni tofauti kabisa na maisha ambayo sisi vijana wa leo tunaishi na mazingira ambayo tunaishi leo ni tofauti kabisa na mazingira ambayo wazee wetu waliishi kwa hiyo kama tunaenda na ufunuo (revelation) ambayo wezee wetu walikua nao tunaweza kushindwa kabisa kutawala mazingira yetu ya leo.

Kuna haja ya kuwa na jitihada za makusudi kutazama mambo ambayo tumefundishwa na wazazi wetu (sisemi ya kuwa wazazi wetu hawakuwa na akili au vitu ambavyo walitufundisha havikuwa vizuri hapana), kitu ambacho nasema hapa ni kuwa baadhi ya vitu ambavyo walitufundisha ni kutokana na uelewa wao wa ulimwengu ambao walikuwa wanaishi kitu ambacho kingekuwa kizuri kama ulimwengu ambao tunaishi sisi ungekuwa kama ulimwengu wao ila kwa sababu ulimwengu ambao tunaishi sio kama ulimwengu wao basi kuna haja za makusudi za kubadili baadhi wa mitizamo ambayo tumejengewa na wazee wetu,(hapa pia simaainishi kubeba kila tamaduni za magharibu ambazo hazijengi)

Bali ninachosema ni kubeba mazuri ambayo tulifundishwa na wazee wetu ambayo yana tija katika ulimwengu wa leo na kuachana na yale ambayo yamepitwa na wakati na pia kuchukua yale mazuri ambayo yanatoka katika ulimwengu wetu wa leo.

Kama tukiendelea kuishi ndoto za wazee wetu basi kuna uwezekano wa kuwa ulimwengu ambao waliishi wao ukawa ulimwengu ambao tunaishi sisi kitu ambacho kitatufanya tuwe nyuma siku zote.

## WEWE NI KABILA GANI?

Sio kitu cha kushangaza kusikia watu wakijigawanya makundi makundi kulingana na makabila yao katika nchi nyingi za afrika ila ulishawahi kujiuliza kabila lina maana gani na nani alianzisha hii kitu?

Naomba unipe muda na uvumilivu ili tuweze kuelewana katika hili

Nimeshuhudia baadhi ya nchi zimegawanyika katika makabila mawili au zaidi kiasi kwamba watu wa kabila hili hawawezi kumpigia kura mgombea wa kabila lile

Kabila ni wazo au falsafa (idea), kama ilivyo ujamaa, ubebari na ideology nyingine ila falsaha ya makabalia imepitwa na wakati ngoja nikuonyeshe.

Mara nyingi watu wanarithi kabila kutoka kwa baba na sio kwa mama, kwa hiyo kama mama ni mchaga na baba ni msukuma basi mara nyingi watoto watajiita wasukuma. Sasa huwa nikikutana na mtu ambaye anajiita yeye ni msukuma au mchaga, mkuyu,mjaluo,muha au kabila lolote lile huwa namuuliza swali moja

### *Aliyeanzisha kabila lako yeye alikuwa kabila gani?*

Kiuhalisia kuna mtu ambaye alianzisha kabila lolote lile (kwani hakuna kabila lililoshuka kutoka mbiguni) na kama watu wanarithi kabila kutoka kwa baba zao je huyu alianzisha kabila lako alikuwa kabila gani?.

Hapa kuna vitu viwili kitu cha kwanza ni kuwa kuna mtu mmoja aliamka asubuhi akasema kuanzia leo tutaitwa waha,wajaluo,wamasai au kabila fulani, na kuanzia siku hiyo watu ambao walikuwa wanazaliwa na huyu mtu wakaanza kujiita kabila hilo na wakaanza kujitenga na watu wengine.

Kifupi mtu mmoja tu aliamua kujitengenezea kabila lake mwenyewe na kama mtu aliamua kujitengenezea kabila lake mwenyewe je mimi leo siwezi kuamua kujitengenezea kabila langu mwenyewe au nikaamua kusema kuanzia leo mimi sina tena kabila?

Je nikiamua kujiita kuwa sina kabila nitakuwa nimekosea kitu gani?

Kitu cha pili ni kuwa kama kabila kila mtu anarithi kutoka kwa baba yake ina maana ya kuwa tunatakiwa kuwe na kabila moja tu duniani, au kusiwe na kabila kabisa na sababu ni hii:

Kama wewe ni mkristo kama mimi unaamini ya kuwa mwanzoni kabisa MUNGU aliumba binadamu wawili (mume na mke) na baada ya hapo kila binadamu anayeishi alizaliwa na hawa binadamu wawili sasa je kama kila mtu anarithi kabila kutoka kwa baba yake na tunafahamu hapo mwanzo baba yetu alikuwa mmoja huoni ya kuwa kutakuwa na kabila moja tu ambalo ni la ADAMU, (kwani kama unarithi kabila kutoka kwa baba yako na baba yako alirithi (inherit) kutoka kwa babu yako tutaenda vivyo hivyo mpaka binadamu wa kwanza kwa hiyo kutakuwa na kabila moja tu, na hili kabila ni sawa na la yule baba yetu wa kwanza), sasa nikuulize swali je ADAMU alikuwa mjaluo?,mchaga?,muha, mkikuyu?, mmasai? Au adamu alikuwa kabila gani?

Hata kama wewe sio mkristo au muislam (ambao tunaamini kiwa binadamu wa kwanza alikuwa adamu)

Hata kama unaamini evolution (mabadiliko ya binadamu), huku nako pia tunaambiwa ya kuwa hapo mwanzo miaka milioni kadhaa iliyopita kulikuwa na mwanadamu wa kwanza ambaye wanadamu wote walitoka kwa huyu kwa hiyo ina maana kama makabila tunarithi kwa baba huku pia kutakuwa na kabila moja.

Kwa hiyo kwa mchanganuo huo tunabaki na sababu moja tu ya kwanini tuna makabila ni kuwa siku moja tu mtu mmoja (babu wa kale) aliamua ya kuwa

kuanzia leo sisi tutakuwa wa kabila fulani, na kama hii ni sahihi je leo hii nini kinanizuia kuanzisha kabila langu?.

Na huyu mtu ambaye alianzisha kabila lako yeye alichagua kutorithi kabila kutoka kwa baba yake kwani kama angeamua kurithi kabila kutoka kwa baba yake basi ingekuwa kama nilivyosema hapo awali ya kuwa kungekuwa na kabila moja kwani sisi binadamu wote tunatoka kwa baba mmoja.

Kuna mtu akasema ya kuwa kabila limetokana na watu kuwa na DNA (Kijinasaba) ambazo zinafanana, nikamjibu ya kuwa hata leo hii ukimchukua mtu mzungu na mwafrika ukawatenga na wakazaa watoto na hao watoto wakawa wanazaana wao kwa wao watakuwa na DNA ambazo zinafanana,

Swali ambalo nilimuuliza ni kuwa je ni ufanano wa asilimia ngapi wa DNA unatosha kumfanya mtu akawa wa kabila la tofauti? Hakuweza kutoa jibu

Je kabila ni kwa sababu mtu anaongea lugha fulani? Kuna baadhi ya watu wanadai ya kuwa kabila la mtu ni kwa sababu anaongea lugha fulani, kifupi hiyo sio sababu (logic) ambayo inafanya watu wajiite kabila fulani kwani kuna watu wanaweza kuongea zaidi ya lugha mbili za kabila tofauti je hao ni kabila gani?

Kuna watu wanadai ya kuwa kabila ni sehemu ambayo umezaliwa na huu ni uongo kwani tunafahamu kuna nchi au mikoa ambayo ina kabila mbili na unakuta watu wamezaliwa sehemu moja, na kama unajiita kabila fulani kutoka na sehemu ambayo umezaliwa je ikitokea watu wawili kutoka mwanza ambao wanajiita wasukuma wakaenda kuishi Dar na wakazaa mtoto ambaye amezaliwa Dar je huyo mtoto atakuwa mzalamo kwa sababu amezaliwa Dar? Jibu ni hapana

Na kuna wengine wanadai kuwa kabila ni tamaduni za sehemu fulani kwa hiyo watu wanajiita wa kabila fulani kwa sababu wana tamaduni za aina fulani huwa nawauliza swali je kama mimi sina tamaduni zozote zile nina haki ya kusema sina kabila? Wanashindwa kujibu

Chukulia umeokota mtoto mdogo (ambaye ni mchaga, ila haukujua wazazi wake wala huyu mtoto anatokea wapi) njiani ukaenda naye katika kijiji ambacho walipo wasukuma akakua na kuwa mtu mzima na anaongea kisukuma vizuri na ana tamaduni za kisukuma kitu gani ambacho kitakufanya ujue kama huyu ni kabila la mchaga? Jibu ni hakuna

Tunarudi mwanzoni ambapo nilisema ya kuwa kabila ni ideology (falsafa), na kwa maoni yangu ni kuwa imepitwa na wakati, binafsi kusema wewe ni kabila fulani haina tofauti na mtu ambaye anasema ya kuwa anaamini katika ubepari au ujamaa kwani zote ni falsafa na binafsi falsafa ya kabila naona haina msingi katika dunia ya leo badala ya kutuunganisha inatugawanya, ulishawahi kusikia nchi ambayo imegawanywa kikabila (na zipo nyingi afrika), sioni sababu ya sisi kugawanywa mpaka kufikia ku uana kwa sababu ya ukabila ni falsafa ambayo imepitwa na wakati.

Hebu fikiria ya kuwa miaka kadhaa iliyopita mzee mmoja ambaye aliishi kipindi tofauti na sisi hakuona utandawazi ambao sisi tumeuona au kuwa na uelewa ambao sisi tunao leo alitengeneza falsafa ambayo inatugawanya sisi ambao tunaishi miaka takribani 200 baada yake (sisemi kwamba wazee watu walifanya kitu kibaya kwani kwa wakati wao ilikuwa sahihi ila kwa sisi ambao tunaishi leo tunahitaji kuwa na kitu kingine bora)

Kama kuna mtu siku moja aliamua kuanzisha kabila je ni nini kinakuzuia leo kuanzisha kabila lako au kusema ya kuwa kuanzia leo mimi sina kabila?

Na kabila maana yake ni nini hasa? Ulishawahi kujiuliza hili au ndio unabeba falsafa ambazo haujui maana yake?.

## KWA NINI USIISHI NDOTO YA WAZAZI WAKO

### STORY

Kuna story niliisikia miaka kadhaa iliyopita ambayo ilinifanya nikawaza mengi

Mzee mmoja katika maisha yake alitamani sana kuwa daktari ila kwa kuwa nyumbani hakukuwa na uwezo wa kumsomesha kuwa daktari akaamua kufanya mambo mengine ila akaapa lazima katika maisha yake atamfanya mtoto wake mmoja kuwa daktari, basi alipozaa mtoto wa kiume akaamua kumpachikia ndoto ya kuwa daktari na akafanya kila ambalo anaweza kumfanya mtoto wake kuwa daktari na kwa sababu sasa ana uwezo wa kumsomesha mtoto wake akaampeleka shule mpaka akamaliza na akafanikiwa kuwa daktari mzuri sana na mzee furaha yake ikawa imetimia.

Sasa siku moja kukawa na sherehe katika hospitali ambayo kijana alikuwa anafanyia kazi na ilikuwa sherehe ya kuwatunukia tuzo wafanyakazi bora kutokana na ufanyaji kazi bora. Sasa moja kati ya watu ambao walikuwa wanapokea tuzo siku hiyo alikuwa huyu kijana basi wazazi wake wakaalikwa na sherehe ikaanza. Kila mmoja akapata nafasi ya kusema kitu ikiwemo wazazi wa huyu kijana, basi kila mmoja akamsifia kijana ya kuwa ni daktari bora, na ana mchango mkubwa sana kwa jamii na ikafika zamu ya wazazi wa kijana na wakafurahi na kusema namna ambavyo wanajisikia faraja kuwa na kijana daktari ilipofika zamu ya kijana kuzungumza alipofika jukwaani akaanza kutoa machozi,

akalia kwa uchungu kila mtu akawa anajiuliza kama haya machozi ni ya furaha au kuna kitu kingine cha ziada, baada ya kulia kwa dakika kadhaa akaanza kuongea

"ni kweli mimi ni daktari mzuri kama mlivyosikia na nina fanya kazi kwa bidii ila kilichonifanya nilie nikuwa udaktari mimi ni kitu ambacho sikipendi mno, toka nikiwa mdogo sikuwa na ndoto ya kuwa daktari ila udaktari ilikuwa ndoto ya baba yangu mimi natamani sana kuwa mwanamuziki na ndio ilikuwa ndoto yangu"

Kijana akaanza kulia tena ikabidi wamtoe pale jukwaani

Wakati wote kijana anaongea haya mzee alikuwa kimya akiwaza ni kwa namna gani ameharibu maisha ya kijana wake, kwani kwa kuwa yeye alitamani kuwa daktari haimaanishi lazima mtoto wake awe daktari kwani kila mtu ana ndoto zake.

Hili linawakumba wengi mno katika jamii za kiafrika na kwa taarifa tu ni kuwa baada ya kijana kuwa na ndoto za kuwa mwanamuziki na kuona zimefeli basi angeamua kumfanya mtoto wake ambaye ana ndoto za kuwa mhandisi (engineer) kuwa mwanamuziki na mchezo unaendelea vivyo hivyo kutoka jamii moja kwenda nyingine.

Kuna baadhi ya watu wanadhani urithi ambayo wanaachiwa na wazazi wao ni mali tu pekee, hapana mfumo wa fikra na ufanyaji mambo ambao wazazi wao walikuwa nao ndio huo huo wanabeba bila kujiuliza kama una tija au la (sasa simaanishi mtoto awe mkaidi kwa wazazi wake, ila unatakiwa ujifunze kufikiri pia)

Na hii sio kwa mzazi na mtoto pekee hii inafanyika kutoka jamii iliyopita kuja jamii inayofuata badala ya kizazi kipya kuwa na mfumo bora wa fikra unakuta kizazi kipya kinafikra na ndoto za kizazi kilichopita

Kama nilivyozungumza katika falsafa ya kwanza ya kuwa unaweza kuchagua maisha ya kutofanikiwa kwa kubeba falsafa ambayo haileti matokeo mazuri kutoka kwa kizazi kilichopita.

Ni hatari kwa kijana wa leo kuwa na mawazo ya mzee wa jana (hasa hasa ambayo hayajengi)

Ukitaka kufanikiwa katika maisha unatakiwa ufikie hatua ya kuanza kufikiri wewe kama wewe unataka nini na unahitaji kuona nini kitokee katika maisha yako kuna baadhi ya ndoto, mawazo (idea,) falsafa (philosopy) ni mzigo kuenda nazo kesho

Live your own dream

Mbele yako na mbele yangu kuna ulimwengu ambao una njia nyingi za uwezekano ambazo hazina kikomo (unlimited possibilities) jukumu lako ni kuiachia akili yako ifikiri na kutengeneza vitu ambavyo inaweza kutengeneza na sio kuishi vitu ambavyo imefundishwa kufanya.

Ujue afrika kwa kiasi kikubwa mawazo ya wengi bado ni ya jana, na wachache wanafikiri mawazo ya leo na baadhi yetu tunafikiri ya kesho

Hapa nina maana kuna watu ambao wanaendeshwa (hawa ndio mawazo yao bado ni ya jana) kuna watu ambao wanajiendesha hawa mawazo yao ni ya leo na

kuwa watu ambao wanaendesha ulimwengu yaani mawazo yao ndio yanaamua ulimwengu uende wapi na ufikiri vipi.

Sio kwamba afrika hakuna watu wenye mawazo ya kuundesha ukimwengu bali wengi bado wanaishi na ndoto za wazee wao hawajui ya kuwa kuna kundi la watu ambao wanatengeneza ndoto ambazo watu wataishi kesho sijui wewe uko katika kundi gani ila mimi ninapenda kwenda kwenye kesho ambayo nimeiandaa mimi.

Wazee wetu (MUNGU awabariki) wengi wao hawakuona ya kuwa kuna uwezekano wa sisi kuwa na athari (impact) ambayo inaweza kuuathiri ulimwengu mzima kwa hiyo wakatupa ndoto ndogo ambayo ina ulimwengu mdogo ya mwanangu nenda shule soma kwa bidii kisha upate kazi na uishi maisha mazuri na wanao, hii ni ndoto nzuri ila ni ndogo mnoo yaani ulimwengu wake ni mdogo sana, kuwa na ndoto ya namna hii katika ulimwengu ambao kuna watu wanamiliki makampuni ambayo yanaingiza mapato makubwa kuliko mapato ya nchi ni kutotendea haki uwezo tulionao

Ni wasaa mzuri sasa wa kuanza kuota ndoto mpya.

Ndoto za wazee watu zilikuwa za ulimwengu mdogo inabidi tuwe na ndoto za ulimwengu mpya

Ni kitu cha kushangaza kuona upande mmoja wa dunia kuna watu wanapigana vita vya makabila au kubaguana kwa sababu ya makabila wakati upande mwingine wa dunia kuna watu wanawaza namna gani ya kubadilisha sayari ya mars kuwa sehemu ambayo binadamu wanaishi, ukisikia utofauti wa fikra ndio huu.

## STORY

Miaka kadhaa iliyopita kijana mmoja alioa mke, sasa siku moja mke wake akakaanga ndizi sasa alipotelewa ndizi mezani kwenye sahani, mume akashangaaa kuona ndizi zote zimekatwa pembeni (yaani mwisho wa kila upande umekatwa), akauliza hii ni stairi gani ya kukaanga ndizi maana sijawahi kuiona, mke akasema nimekua naona mama anapika hivi, kwa kuwa mama alikuwa hai ikabidi wachukue simu wamuulize eti mama mbona ulivyokuwa unakaanga ndizi ulikuwa unakata ndizi kila pembe, mama akajibu sijui hata mimi niliona mama anapika na nilivyokuwa mkubwa nikawa napika vivyo hivyo, sasa bahati nzuri mama wa mama (yaani bibi wa mke naye alikuwa hai), basi siku moja wakamualika mama pamoja na bibi katika sherehe ya krismasi na wakiwa mezani bibi akaulizwa eti bibi kwa nini ulikuwa ukikaanga ndizi unazikata pembeni?

Bibi akajibu kikaango changu kilikuwa kidogo kwa hiyo ndizi nzima ilikuwa haienei kwa hiyo ikanibidi niwe napunguza ndizi kwa kuikata pembeni, familia nzima ikaangua kicheko.

Maana mama alivyoona ndizi inakatwa pembeni akajua ndio stairi ya upikaji na yeye akawa anapika vivyo hivyo, mtoto naye akabeba stairi ya kukata ndizi pembeni, mpaka siku mumewe alipouliza ndio akili ikafunguka kuwa kukata ndizi pembeni sio stairi ya upikaji bali bibi alimua kukata kwa sababu alikuwa na kikaango kidogo.

Kuna wakati watu wanabeba fikra au kitu bila kujiuliza kimetokea wapi, unatakiwa kujiuliza je kwa nini tunafanya hivi na sio vile au kwa nini tunaamini hivi na sio vile na sio kubeba ndoto au falsafa bila kujua imetokea wapi

Kuna baadhi ya vitu kama makabila na imani nyingine ukijiuliza zimetokea wapi unaacha kushikamana nazo kwani msingi wake haupo.

Kinachoangusha afrika ni falsafa yake.

# FALSAFA YA 9

## SAFARI MOJA HUANZISHA NYINGINE

Maisha siku zote yanategemea mzani uliopo kati ya vitu viwili ambavyo vipo katika pande mbili na ukitaka kufanikiwa ni vyema kulijua hili ya kuwa siku zote ukitaka kufanikiwa hautakiwi kuelemea upande mmoja wa kitu na kuacha upande mwingine.

Katika safari ya maisha kuna makundi ya aina tatu

1) Kundi la kwanza ni watu ambao hawawezi kuanza kitu mpaka kila kitu ambacho kinahitajika kiwepo
2) Kundi la pili ni kundi ambalo wao huanza safari bila kuwa na kitu chochote
3) Kundi la tatu ni kundi ambalo huwa na taarifa kiasi na wanaanza safari

Makundi mawili ya kwanza mara nyingi huwa yanashida kwani wale ambao wanasubiri kupata kila wanachohitaji au taarifa zote kabla ya kuanza safari mara nyingi huwa hawaanzi safari kabisa kwani ni ngumu kuwa na taarifa za kila kitu kwa kipindi ambacho unakuwa unaanza.

Kundi la pili huwa wanaanza safari bila kuwa na taarifa ya aina yoyote ile na mwisho wa siku inawachukua muda mwingi kuzunguka eneo moja au kujua wafanye nini.

Kundi la tatu ndio kundi ambalo unatakiwa kuwa

Siku zote ukianza safari moja katika maisha unapata kujifunza ni nini kinawezakana na nini ambacho kinahitajika ili uweze kufanikiwa na haya mengi utajifunza sio ukiwa nyumbani bali ukianza safari ndio utaona baadhi ya njia huko mbele na sio ukiwa nyumbani.

**MFANO**

Kuna jamaa mmoja alikuwa ana elimu ya kitu fulani kwa undani na alikuwa anaweza kufundisha ila changamoto alikuwa hajui anaweza vipi kuitumia elimu yake kuwafikia watu wengi kwani hata kama akiandika kitabu hakuna mtu ambaye atanunua kitabu cha mtu ambaye hamfahamu, kwa hiyo alichokifanya alikuwa katika kundi moja la whatsapp ambalo lilikuwa linahusiana na kitu alichokuwa anakifahamu, akawa anaandika makala fupi fupi kuhusu mada anayoifahamu kwa kuwa alikuwa na uelewa wa kutosha na uwezo wa kufundisha basi akawa anapata watu wakusoma na kuuliza maswali mbali mbali na kupitia maswali ambayo alikuwa anaulizwa akajifunza vitu viwili , kwanza ni kutafuta majibu ya vitu ambavyo alikuwa hafahamu na pili kujua ni vitu gani ambavyo watu walikuwa wanahitaji kufahamu (kwani ukiwa kama mwandishi ni sawa na mfanya biashara unaandika kitu ambacho watu wanahitaji na sio kitu ambacho unakijua ambacho hakina uhitaji).

Basi baada ya kuanza safari ya kuandika makala akapata wazo kulingana na muitikio wa watu ya kuwa anaweza kuandika vitabu vifupi vifupi kwa nakala laini ( softcopy) na kuanza kuuza kwa wale watu ambao wanamfahamu hasa hasa kwa lile kundi la whatsapp ambalo alikuwa anafundisha na akafanikiwa kufanya hivyo na akawa anapata pesa kidogo kidogo na siku moja katika pitapita akakutana na

tovuti moja ambayo inauza vitabu mtandaoni ambayo anaweza kuandika vitabu kwa nakala laini akauza kwa wateja wengi wale ambao anawafahamu na wale ambao hawafahamu, na akafanya hivyo na akawa anapata wateja, sasa moja kati ya wasomaji wake akawa amependa uandishi wa huyu jamaa na vitabu vyake na yeye alikuwa na pesa kidogo na pia anafahamu baadhi ya watu ambao wanafanya biashara ya kuuza vitabu, akaamua kukaa chini na kuongea na jamaa na akajitolea kutoa vitabu vyote vya jamaa kwa mfumo wa nakala ngumu (hardcopy) na kuwa anauza kwa makubaliano ya kuwa asilimia 30 ya mauzo itachukuliwa na huyu anayetoa vitabu na asilimia 70 itaenda kwa mwandishi wakakubaliana kazi ikaanza.

Vitabu vya jamaa vikawa maarufu sana kwa watu wa nchi ile kwani alikuwa anaandika kwa lugha nyepesi yenye kueleweka kwa watu wengi na baadhi ya watu wakawa wanamualika kufundisha katika mikutano ya kulipwa.

Muda si muda kwa kuwa sasa ni maarufu na ana pesa akaamua kuanzisha kampuni yake mwenyewe ambayo aliitumia kuuza baadhi ya mafundisho kwa mfumo wa video na sauti na pia kuandaa mikutano kwa ajili ya kufundisha na kutokea hapo akaajiri watu kwa ajili ya kufundisha na kuuza vitabu na yeye akaenda kufanya mambo mengine na biashara ikawa inaendelea.

Katika mfano wetu nadhani umejifunza kitu kimoja ya kuwa ni safari ya kwanza ya kuandika makala katika kundi la whatsapp ndio ilimfanya huyu jamaa akaanza safari nyingine baada ya nyingine na hata kufikia kuwa na kampuni yake mwenyewe.

Kuna baadhi ya safari za kuelekea mafanikio yako unaweza kuzianzisha pale tuna ambapo unakuwa safarini na sio ukiwa hujaanza safari kwa hiyo ni muhimu sana

ujifunze kuanzisha safari hata kama taarifa ambazo unazo hazitoshi kwani safari moja huwa inaangaza njia ya safari nyingine.

Popote pale ambapo unadhani unaweza kuanzia anzia hapo hapo usisubiri mwanzo mkamilifu (perfect start), kwani huu mwanzo wa aina hii haupo.

Katika baadhi ya vitu ambavyo nimeona mchango wake katika kunifikisha hapa nilipo ni huu muujiza wa kuanza safari popote pale ambapo naona inawezekana kuanza safari kwani kuna baadhi ya mafanikio hauwezi kukutana nayo mpaka unapokuwa safarini.

## MFANO

Miaka kadhaa iliyopita wakati nikiwa mwanafunzi wa chuo mwaka wa 3, nilitamani sana kuwa na kiwanja changu mwenyewe na nikakusanya pesa ambayo nilikuwa nayo ambayo nilipewa na serikali kama mkopo nikaanza safari ya kutafuta kiwanja nilikuwa na jumla ya kama laki 8, nikatoka siku moja wikiendi kwenda kutafuta eneo la kununua, nilivyotoka nikakutana na kijana mmoja ambaye alikuwa anafyatua matofali na nikampa kazi ya kutafuta eneo la kiwanja.

Baada ya muda akaniambia amepata kiwanja nikaenda nikaona kinafaa na nikanunua kile kiwanja kwa bei ya laki 5 na pamoja na gharama nyingine nikabaki na kama laki moja na nusu.

Sasa baada ya kupita siku kadhaa nikaenda kuangalia kiwanja ambacho nimenunua nilipo karibia na kiwanja changu nikakutana na bibi ambaye aliniuliza unaenda wapi kwani aliniona ya kuwa ni mgeni wa eneo lile nikamwambia kuwa nimenunua kiwanja maeneo haya, akaniambia na yeye ana kiwanja anauza na nikaomba kwenda kuona hicho kiwanja nilipofika akaniambia

kuwa kiwanja anauza laki 5 pia, tukabishana bei mpaka ikafika laki tatu na ishirini, kwa kuwa sikuwa na pesa nikaomba mama aniongezee pesa na nikanunua hiki kiwanja pia, kwa hiyo jumla sasa nilikuwa na viwanja viwili.

Baada ya kumaliza chuo nikapata hela kidogo na kuanza kujenga (kwanza baada tu ya kumiliki kiwanja uelewa wangu ukabadilika nikawa na mawazo ya kujenga kitu ambacho nisingekuwa nacho kama nisingekuwa na kiwanja), wakati naanza kujenga nikakutana na fundi ambaye alikuwa moja kati ya viongozi wa eneo lile na akaniambia ya kuwa kuna maeneo ambayo yanauzwa na unaweza kununua kwa ajili ya kuchimba madini ya ujenzi, akanieleza biashara inavyoenda na nikanunua maeneo kadhaa, baada ya kununua ikapita miezi kadhaa na tukaanza kazi ya uchimbaji na nikaanza kuingiza pesa ambayo sikudhani kama ningeipata kwa muda mfupi, kwani hii biashara ilikuwa na faida mno.

Yote haya yameanza baada ya kuwa mimi kuanza safari ya kutafuta kiwanja kama mwanafunzi enzi hizo, na kipindi naanza kutafuta kiwanja nilikuwa sina pesa hata senti moja ila nilitafuta ili nijue viwanja vinauzwa bei gani eneo lile na kwa kufanya hivyo nikajua kuwa ninaweza kupata kiwanja kwa laki 5 na ndio nikaamua kutumia pesa ya mkopo ambayo safari hii iliniletea kiwanja, nyumba, biashara na viwanja vingine vingi baadae.

Kama nisingeanza ile safari fupi nisingeweza kufika hapa nilipo

Ukianza safari moja achana na kuwa utajifunza mengi njiani pia uelewa wako utabadilika na huu uelewa mpya unakuwezesha kuona fursa mpya ambazo usingeweza kuziona kama usingeanza safari ya kwanza

Pia utajenga mahusiano mapya na watu wapya ambao pia watakuwa chachu ya kukufungulia safari nyingine.

Jaribu kufikiria ni milango mingapi inaweza kufunguka kama ukiamua kufuata njia ambayo unaiona mbele yako?

Kuna wakati watu wanasubiri kuona picha nzima ya kitu ndio waanze safari kitu ambacho kinaweza kuwa kosa kwani unapoanza unakuwa hauna uwezo wa kuona picha nzima ya kitu hata kama mtu akikuonyesha hiyo picha kwani ili uweze kuona picha mzima ya kitu lazima uwe na uelewa wa suala zima lililoko mbele yako kitu ambacho ni kigumu kwa wale watu ambao bado ndio wanaanza safari ila kwa kuanza kutembea unapata kujua baadhi ya mambo na hayo yanafungua milango mipya na kabla haujajua nini kimetokea unajikuta uko mbali zaidi ya pale ambapo ungekuwepo leo.

## ACTION BEAT INA ACTION

Ukichunguza maisha ya binadamu ni kuwa kitu ambacho unafanya na kitu ambacho haufanyi vyote vina mchango wa kuyapeleka maisha yako mbele (both action and inaction have contribution to your life).

Yaani maisha yako yalipo leo mchango wa vitu ambavyo unafanya na vitu ambavyo haufanyi

Your today life is combination of the things that you do and the things that you do not do

Ila matendo au vitu ambavyo unafanya vina mchango mkubwa katika maisha yako kuliko vitu vile ambavyo haufanyi.

## MFANO

Kama haujaiba au kufanya kitu ambacho kitafanya ustahili kwenda jela basi utafurahia maisha yako uraiani, kama unafanya kazi na unaingiza kipato basi utaishi maisha mazuri uraiani

Hapo unaweza kuona ya kuwa vitu ambavyo haufanyi na vitu ambavyo unafanya vyote vina mchango wa kukuweka hapo ulipo,

Ni kwa sababu huibi au kufanya kitu ambacho kinastahili kukupeleka jela (inaction) ndio maana uko mtaani, pia ni kwa sababu unafanya kazi ndio maana una maisha mazuri (action).

Kwa hiyo unaweza kuona vyote kufanya kitu na kutofanya kumechangia wewe kuwa hapo.

Unaweza kupokea matokeo mazuri kwa kutokufanya kitu na unaweza kupokea matokeo kwa kufanya kitu, ila mtu ambaye anafanya kitu anakuwa na matokeo mazuri kuliko yule ambaye hafanyi kitu kwani katika kufanya kitu unajifunza vitu vipya na unapokuwa na uelewa mpya unapata kuona vitu vingine zaidi ambavyo usingeweza kuviona kama usingeanza safari.

Ukikaa na mtu yoyote ambaye amefanikiwa na kuzungumza naye basi hiki kitu ambacho tunakizungumza hapa utaona kuwa ndicho kimefanya wengi wakafanikiwa na wengine kushindwa, wale waliochagua kufuata njia ndogo ambayo iko mbele walijikuta wakiona njia nyingine mbele yao na kuziendea na hatimaye kufika pale ambapo walipo leo wakati wengine ambao walikuwa wamekaa tuu wakisubiri mwanzo uliokamilika hawana kitu.

Hata ukichunguza maisha yako utagundua ya kuwa kuna baadhi ya vitu usingekuwa navyo leo kama usingeanza ile safari ndogo ambayo ulikuwa hauoni mwisho wake ila ulipoanza safari ukakutana na njia nyingine ambayo

ikakupeleka katika eneo jingine na kabla haujajua nini kinaendelea ukajikuta una mafanikio ambayo usingeweza kuyapata kama usingeanza safari wakati ule.

Unachokiona mbele yako ni kila kitu kilichoko mbele yako kama unaona hakiwezi kukufikisha unakotaka kwenda basi unachotakiwa kufanya ni kutembea mbele kidogo utaweza kuona kitu tofauti na unachokiona leo na kati ya vitu vipya ambavyo unaviona kimoja wapo kinaweza kuwa ndio njia sahihi ambayo ulikuwa unaihitaji ila kama ukiendelea kukaa hapo ulipo hakuna kitu tofauti ambacho utakiona. Pointi yangu ni fanya kitu kwa hali unayoiona leo usisubiri mpaka kila kitu kiwe perfect

Kuna kitu cha ajabu katika kuanza safari, kwani unapoanza safari moja huwa haishii kuwa moja bali inafungua safari nyingine na safari nyingine inafungua safari mpya kabla haujajua unajikuta umekaa katika mafanikio ambayo haukutegemea kuyafikia.


Jifunze hili ya kuwa kuanza safari ni bora kuliko kusubiri kuanza safari ambayo ni kamilifu (perfect).

Kama ukiweka falsasa hii katika maisha yako ndani ya miaka kadhaa utarudi na ushuhuda ambao utakushangaza hata wewe.

Hili suala hata watu wanaotengeneza bidhaa wanalifahamu ya kuwa kuliko kukaa chini na kutengeneza bidhaa ambayo imekamilika ambayo hawajui kama itakubalika sokoni wanaanza na kutengeneza bidhaa ambayo ni ya kawaida wanaiita MVP ( minimum viable product) na wanaiweka sokoni na kuangalia muitikio wa watumiaji wanapo pokea taarifa mpya wanabadili na kurekebisha vile vitu ambavyo wanadhani vinahitaji mabadiliko na taratibu wanatengeneza bidhaa bora, karibuni bidhaa nyingi unazoziona sokoni zinafanya vizuri zilianza kwa mtindo huu, na uzuri wa mfumo huu ni kuwa kama bidhaa sio nzuri basi inatolewa sokoni mara moja kabla haijamuingiza gharama kubwa mtengenezaji.

Fikiri kama bidhaa zinatengenezwa kwa namna hii si zaidi sana wewe kuendesha maisha kwa mfano huu pale ambapo unaona unahitaji kufanya kitu lakini mwanga ulionao hautoshi?

PATA NAKALA NZIMA YA KITABU



**©Maombi A. Chagamba**

**Simu: +255713999596,**

**+255752102169**

**WhatsApp:**

**+255713999596**

**Email [wiseinvestorr@gmail.com](mailto:wiseinvestorr@gmail.com)**


MAMBO 9
UNAYOTAKIWA KUJUA
KUHUSU
KUNENA
KWA LUGHA
Na jinsi unavyoweza kuanza
kunena kwa lugha
Maombi Abel chagamba